# 1. BWANA MARINGO

Katika Nchi ya Ajabu kuna bwana mmoja ambaye maringo yake yamevuka mpaka.

Bwana huyo kwa kawaida anajipenda sana, hasa kwa mavazi. Utamwona leo amevaa shati hili na suruali hii. Kesho atabadili nguo zingine. Hivyo hivyo, kiasi cha kuonekana maridadi hasa.

Kwa upande wa maringo ni kwamba hata anapotembea hujiburuzaburuza kwa madaha mengi. Anapotupa mguu mmoja mbele husimama kidogo ndipo atupe na mguu wa pili!

Tabia yake hiyo ya kutembea kwa maringo mara nyingi inamhatarisha endapo itatokea hatari yoyote na kumkabili kama vile moto au wawindaji. Wenyeji wamempachika jina na kumwita 'Bwana Maringo', ingawa ana jina lake halisi!!

Swali: Jina lake halisi ni lipi?





## 2. MBUZI MTIIFU

Katika Nchi hiyo ya Ajabu anaishi mbuzi mmoja wa ajabu mno. Mbuzi huyo kwa kawaida hali majani katu. Chakula chake daima ni maji. Lakini hata hayo maji anayanywa kwa namna ya kushangaza sana.

Unapomchukua kwenda naye kisimani ili akanywe maji, anapofika hapo kisimani kabla ya kuanza kuyanywa hayo maji atakuambia, "Tafadhali nishike mkiani ili ninywe maji."

Ukimshika mkiani mbuzi huyo hujituliza na kuwa mpole na mtii mno. Basi hapo atatumbukiza kichwa chake majini na kujaza funda tele. Sasa la ajabu ni kwamba maji hayo atakayoyajaza kinywani hatayanywa, badala yake atayatema nje ya kisima! Atafanya hivyo mpaka hapo utakapochoka kuushika huo mkia na kuamua kurudi nyumbani!

**Swali:** Mbuzi huyo anaitwaje?





## 3. MWANAMAJI

Katika Nchi ya Ajabu anaishi mtu mmoja wa ajabu sana. Badala ya kuishi na wenzake katika nchi kavu, mtu huyo ameamua kuishi yeye na jamaa zake mbali na watu wengine.

Jambo la kushangaza ni kuwa mtu huyo si





kwamba tu amejitenga na wenzake, bali pia ni kule kuamua kwenda kuishi majini!

Muda mrefu wa maisha yake pamoja na jamaa zake huishi ndani ya maji. Ni mara chachechache tu ndipo utawaona wakiwa nchi kavu. Mara nyingi utawaona wakiwa kwenye kingo za mito ama visima ama mabwawa na vidimbwi wakiota jua.

Anapoulizwa kwa nini ameamua kwenda kuishi ndani ya maji, mtu huyo hujibu, "Watu wote wananicheka mimi, mke wangu na watoto wangu kwamba ati tunanuka! Ati wachafu hatuogi wala hatufui. Sasa tumeamua kuishi majini ili tutakate: nguo zetu na miili yetu."

Cha kushangaza ni kwamba licha ya huko kuoga mchana na usiku, mwanamaji huyo pamoja na jamaa zake bado wanatia kinyaa ukiwatazama, kwani bado wanaonekana wachafu kuliko hata juzi na jana!

**Swali:** Mtu huyo anaitwaje?

# 4. MPISHI ASIYENENEPA

Ni kawaida ya wapishi wengi kunenepa. Ni mara chache kumwona mpishi amekondeana miaka nenda miaka rudi akiwa katika kazi hiyo.

Mpishi wa mfalme mara kwa mara hupika vyakula vizuri vizuri kama vile ndizi, wali na vitoweo kama nyama, samaki na mboga aina kwa aina. Mpishi kama huyo ana kila sababu ya kunenepa kwa maana mapishi yote hayo huanzia kwake kwa kuyaonja na hata shibe kamili.

Lakini katika Nchi ya Ajabu, mpishi wa mfalme anamshangaza kila mtu. Mpishi huyo hanenepi miaka yote licha ya vinono visivyokuwa na idadi anavyokula hapo jikoni!

Baadhi ya watu wanaamini kuwa sababu inayomfanya mpishi huyo asinenepe ni kwamba daima hula chakula hapo jikoni penye fukuto kali la moto. Wanasema kwamba kama angekuwa anachukua vyakula hivyo na kwenda kulia kivulini basi angenenepa tu!

**Swali:** Je, mpishi huyo anaitwaje?





## 5. TABIA TOFAUTI

Katika Nchi ya Ajabu nilikutana na familia moja ya ajabu. Familia hiyo ni ya watu watatu, yaani baba, mama na mtoto. Wote watatu wana tabia zilizohitilafiana.

Baba ana tabia ya ukali. Ni mkali sana hata kama akijiwa na mgeni hana muda mrefu atamkorofisha. Atamchemsha kwa kumfokea na kuuweka moyo wa mgeni huyo katika joto kali!


Tofauti na baba huyo, mama, yaani mkewe, ana tabia ya upole daima.

Mtoto naye je?

Mtoto ndiye kichaa! Hatulii nyumbani asilani. Nyakati zingine anapoona chakula kinapikwa yeye hutoweka na kutokomea mitaani. Hata anapofungiwa milango ili asitoke angoje chakula, yeye kwake ni bure tu. Atatoka atatoka tu, hata kama ni kupitia madirishani ama darini!!!

**Swali:** Baba anaitwaje, mama anaitwaje na mtoto anaitwaje?






## 6. BLANKETI LA MUNGU!

Haya tena, maajabu mengine!

Ukipata bahati ya kufika katika hiyo Nchi ya Ajabu utaonyeshwa blanketi moja kubwa sana lililotandazwa.

Cha ajabu utakachokiona kwenye blanketi hilo ni chawa. Chawa hao ni wengi mno na wako katika ukubwa tofauti.

Kingine cha ajabu ni kwamba chawa hao hawaonekani mchana hata kama macho yako





yana uwezo mkubwa vipi wa kuona! Na hata ukitumia darubini ni kazi bure, hutawaona!

Inasemekana kwamba chawa hao hukimbilia msituni kwenda kujificha mapema tu kunapopambazuka. Jioni giza linapoingia ndipo chawa hao hutoka mafichoni kwao na kulivamia hilo blanketi!

Ajabu nyingine ya chawa hao ni kwamba nyakati hizo za usiku wa giza kila mmoja hutoa mwanga na kuonekana kwa uwazi kabisa!

Wenyeji hawajishughulishi kuwaua chawa hao kwani hawana madhara. Hata siku moja chawa hao hawajapata kugusa blanketi ama nguo yoyote ya mwanadamu bali tu hilo blanketi kubwa ambalo wenyeji wanasema kwamba blanketi hilo ni mali ya Mungu!

**Swali:** Chawa hao wanaitwaje?

## 7. BUBU ANAYECHEKESHA!

Katika Nchi ya Ajabu anaishi mtu mmoja wa ajabu. Mtu huyo ni bubu. Hasemi na mtu bali hujaribu kila vilivyo kumwigiza hapo kwa hapo mtu mwingine yeyote anayetokea kumwandama.





Kwa kawaida bubu huyo huandamana na mtu yeyote hata kama safari ya mtu huyo ni ndefu vipi! Tena hachoki kutembea. Ukiamua kusimama ama kuketi ili kupumzika, naye ataamua hivyo hivyo!


Bubu huyo hataondoka nyuma yako hata kama utamkaripia. Kwanza yeye hatakujibu! Pengine atakuona mjinga! Na kama utamgeukia na kumkurupusha, basi kila unavyokimbia naye hukimbia kasi hiyo hiyo. Ukibandika unyayo mbele, naye hapo hapo hubandika unyayo wake! Aidha kama utaamua kumkimbia basi naye hukukimbiza! Ukisimama naye husimama! Ukimtupia ngumi naye hukuigiza hapo hapo kwa kutupa ngumi yake! Lakini ukikohoa au kumsemesha naye hatasema neno, atakutazama tu!

**Swali:** Bubu huyo anaitwaje?

## 8. NG'OMBE WA AJABU!

Kama siku moja utapata bahati ya kuitembelea hiyo Nchi ya Ajabu, bila shaka utashangazwa sana na ng'ombe wa huko.

Kwa kawaida ng'ombe tunaowajua sisi huku kwetu ni wale wanaotoa maziwa kwa nyakati tu wanapokuwa na watoto, yaani ndama. Ni nyakati hizo tu ambapo ndama





hunyonya maziwa na hapo hapo binadamu huwakamua ng'ombe hao na kujipatia maziwa.

Lakini ajabu ya nchi hiyo ya wenzetu ni kwamba ng'ombe wa huko hutoa maziwa nyakati zote. Yaani hata kama hawana watoto maziwa hupatikana tu kila wanapokamuliwa!

Jambo jingine la ajabu ni kwamba maziwa ya ng'ombe hao wa ajabu hayanywewi na kiumbe yeyote! Matumizi makubwa ya maziwa hayo ni kutengeneza vitu katika viwanda kama vile mipira ya ndani ya baiskeli, motokaa na kadhalika.

Tabia ya ng'ombe hao wa ajabu ni kwamba hawakai katika mazizi kama ng'ombe wetu. Wao huishi porini wakijilisha wenyewe. Na ajabu ni kuwa vyakula wanavyokula viko chini ardhini, na huvila kwa kutumia miguu yao!

Swali: Je, ng'ombe hao wanaitwaje?

## 9. NDEGE WA AJABU!

Je, umepata kumwona ndege wa ajabu? Basi katika hiyo Nchi ya Ajabu kuna maajabu ya ndege mmoja ambaye kwa bahati mbaya jina lake nimelisahau.

Haya, ni maajabu gani ya ndege huyo?

Maajabu ya ndege huyo ni kwamba anapopaa angani huwa mkubwa ajabu! Hututumka mwili wote na kuwa kitu cha kutisha sana. Mbawa zake hutanuka na kufanya mduara mkubwa mithili ya ungo mpana!

Cha kushangaza ni kwamba ndege huyo anaporudi chini hujikunyata na kuwa mdogo na mwembamba kama bakora tu!

Mara nyingi ndege huyo hupaa angani akiona mvua. Kutokana na upana wa mbawa zake, ndege huyo huwasitiri binadamu walioko chini yake kwa kutonyeshewa na mvua. Ndege huyo ni rafiki mkubwa wa binadamu kwani huishi nao katika majumba yao!

**Swali:** Ndege huyo anaitwaje?





## 10. KABILA KALI

Kuna kabila moja kali sana katika hiyo Nchi ya Ajabu. Ukali wa watu wa kabila hilo huanzia wanapopata makamo makubwa kiasi. Wakati wanapokuwa wachanga ama watoto wadogo bado huwa wapole mno hata hawamudu kumdhuru mtu. Hivyo kutokana na uchanga na upole huo watu huwaonea kila mara kwa kuwaparura kwa mapanga.

Watu hao huwa hivyo kwa muda wote huo wa kuwa watoto, lakini mara tu wanapopevuka hukumbuka mabaya yote waliyotendewa. Kwa hivi kazi yao sasa inakuwa ni kulipa kisasi. Hufanya hivyo kwa kuwadunga maadui zao sindano zisizokuwa na dawa!

Mara nyingi sindano hizo hudungwa kwenye nyayo za miguu na kusababisha majeraha makali pamoja na kuvimba. Inasemekana kuwa hata kama wamekufa siku nyingi lakini bado tu watazitega hizo sindano na kuwadhuru maadui zao!

**Swali:** Watu hao wanaitwaje?





# 11. MFUNGWA WA MAPENZI

Katika Nchi ya Ajabu anaishi mama mmoja mwenye mapenzi mengi mno kwa watoto wake. Lakini kutokana na utukutu wa watoto wake, mara nyingi wamewahi kufungwa gerezani.

Mama huyo kila ilipotokea kifungo kwa mtoto wake mmoja au hata ni wote, basi naye huenda serikalini na kuomba ama kulazimisha naye afungwe gerezani ili apate kuishi na watoto wake hao!

Kufuatana na sheria za Nchi ya Ajabu, mama huyo kila mara alikubaliwa kwenda kuishi huko gerezani pamoja na watoto wake hadi hapo watakapomaliza muda wa kifungo. Huko gerezani mara nyingi mama huyo anakuwa na kazi moja tu ambayo ni kuwakumbatia watoto wake!

**Swali:** Mama huyo ni nani na hao watoto ni akina nani?





## 12. WAKISAFIRI HAWARUDI!

Katika hiyo Nchi ya Ajabu kuna kikundi cha watu ambao ni wasafiri. Bila ya shaka ni wafanyabiashara.

Masikani yao hasa ni angani! Watu hao husafiri kutoka nchi yao hadi dhini mara moja ama mbili kwa mwaka.


Kwa kawaida wasafiri hao hufanya safari zao wakiwa na umri mpevu mao. Mara nyingi huanza safari wawapo mahututi wa kukata roho!

Wakati wanapokuwa na umri mdogo watu hao hufanya kazi za nguvu na kujitosheleza kwa kila kitu. Mtu yeyote angeweza kufikiria kwamba hawataondokewa na nguvu za kiafya na za kiuwezo.

Lakini cha ajabu ni kwamba wakati ukifika watu hao hujiona wanyonge wa afya na kuamua kusafiri ili wakafe mbali nanchi yao! Labda wanaona aibu kufia katika nchi yao!

**Swali:** Wasafiri hao huitwaje?





## 13. MNYAMA ANAYEOGOPA JUA!

Katika Nchi ya Ajabu anaishi mnyama mmoja wa ajabu.

Mnyama huyo siku zote huomba kwa Mungu ili jua lisitoke. Yeye rafiki yake





mkubwa ni mvua tu hapa duniani. Kila siku huomba dua ili mvua inyeshe!

Mnyama huyo huwaudhi mno wanadamu kila anapotembelewa na huyo rafiki yake, mvua. Ana mchezo mmoja mbaya na wa hatari sana anaowafanyia hao wanadamu. Utamwona nyakati zote amejificha sehemu wanazopita wanadamu.

Wanadamu wanapomkaribia mnyama huyo mahali alipojificha, basi hapo hapo mnyama huyo humpiga mweleka mtu mmoja mmoja. Wapende wasipende watu hao watadondoka chini na kutapakaa matope. Wakati mwingine mieleka hiyo huwavunja watu viungo vyao vya miili. Pengine mtu avunjike mguu, mkono na kadhalika.

Kila watu walivyomwinda mnyama huyo wamwue wameshindwa. Dawa pekee ni kuanza kumfukuza huyo rafiki yake, yaani mvua. Halafu kuliita jua limshambulie mnyama huyo kwa kumchoma na moto wake mkali!

**Swali:** Mnyama huyo anaitwaje?

## 14. RAFIKI MPAKA KABURINI!

Katika hiyo Nchi ya Ajabu wanaishi aina fulani ya wanyama ambao wana maajabu makubwa mno. Wanyama hao wamefanya maajabu kwa namna wanavyowapenda mno binadamu.





Maajabu ya upendo wa wanyama hao ni kuwa kuanzia binadamu anapozaliwa tu, hata siku hiyo hiyo ya kwanza, hujisogeza kwa furaha mahali alipo mtoto na kuomba ruhusa kwa mkunga ili wapate kumkumbatia huyo mtoto!

Wanyama hao wanapopewa idhini basi kuanzia hapo hawatataka tena kuondokana na mtoto huyo. Watafanya kila wawezavyo ili kumstiri mtoto huyo kutokana na baridi. Na mara nyingi humkumbatia mtoto huyo ili watu wengine wasiweze kuuona mwili wote wa mtoto.

Kwa kawaida marafiki hao huendelea kuishi na wanadamu katika maisha yote ya duniani. Kwa idadi marafiki hao ni wengi kuliko wanadamu. Wakati mwingine wanyama hao wanaweza kuwa zaidi ya kumi wakimhudumia binadamu mmoja, usiku na mchana wakipeana zamu.

Lakini la mwisho la ajabu kwa wanyama hao marafiki ni kwamba hata siku ya binadamu anapofariki dunia, mmoja wao hujitolea ilimradi azikwe pamoja na binadamu huyo!

**Swali:** Wanyama hao wanaitwaje?

## MAJIBU YA KITABU CHA KWANZA

1. Kobe/Konokono.
2. Sindano.
3. Vidole na ugali.
4. Kinoo.
5. Firigisi.
6. Uyoga.
7. Chungu/Sufuria.
8. Nguzo za umeme/simu.
9. Nguzo za nyumba.
10. Saa.
11. Mwangwi.
12. Muhogo.
13. Kitanda.
14. Mgomba.



COLUMBIA UNIVERSITY
0029403812

MRADI WA VITABU VYA
WATOTO TANZANIA

# VITENDAWILI KWA HADITHI

## KITABU CHA PILI



J. Mkabarah